# Nafasi ya Fasihi katika Kusawiri suala la Dini

Alfred Malugu

**Ikisiri**

*Makala haya yanatalii maana ya dini na pia, yanatalii kazi sita za fasihi jinsi zinavyolisawiri suala zima la dini kwa njia ambayo inatufanya tuhoji ni ipi nafasi ya dini kwa mwanadamu? Na je, ni kweli dini ni asasi timilifu kama ambavyo imekuwa ikichukuliwa na wanajamii? Haya ni baadhi tu ya maswali yaliyochochea uandishi wa makala haya. Hivyo basi, ili kujibu maswali hayo, makala haya yatazitalii kazi za waandishi watano ambao ni Ngugi Wa Thiong'o, Farouk Topan, Euphrase Kezilahabi[1], Ebrahim Hussein na Chinua Achebe kuhusiana na jinsi walivyolisawiri suala hili la dini na jinsi linavyotuibulia maswali hayo yaliyoulizwa hapo awali. Kazi zitakazohusika katika makala haya ni The Black Hermit (Mtawa Mweusi), Things Fall Apart (Shujaa Okonkwo), Rosa Mistika, Mfalme Juha, Aliyeonja Pepo na Kwenye Ukingo wa Thim.*

## 1.0 Utangulizi

Kupitia vitabu mbalimbali vya fasihi, ni dhahiri kuwa waandishi mbalimbali wamesawiri suala la dini katika kazi zao. Hata hivyo, usawiri wa suala hili la dini umetofautiana kati ya mwandishi mmoja hadi mwingine na tena hata baina ya kazi moja na nyingine. Suala la dini limesawiriwa kwa namna mbalimbali; chanya na hasi. Aidha, inaonekana kwamba suala hili la usawiri wa dini na jinsi linavyojitokeza katika kazi za fasihi limeshughulikiwa zaidi na wahakiki katika kazi za Euphrase Kezilahabi huku kazi nyingine za kifasihi zinazosawiri suala hilo hilo la dini zikionekana kusahaulika. Euphrase Kezilahabi ni miongoni mwa waandishi wanaosemekana kulisawiri suala la dini ya Kikristo kwa kupitia imani ya Kikatoliki kwa njia mbalimbali ikiwemo njia ya kejeli[2]. Kwa hiyo, makala haya yanakusudia kumakinika na jinsi suala la dini ya Kikristo na Kiislamu linavyosawiriwa kwa kupitia kazi sita za fasihi zilizoorodheshwa hapo juu.

---

[1] Tumetumia kazi moja ya Euphrase Kezilahabi kushadidia kile kilichokuwa kikisemwa kuwa Kezilahabi ni mwandishi aliyelisawiri suala la dini kwa namna ya kukejeli asasi ya dini hususani imani ya Kikatoliki. Hapa tumetumia kazi yake moja kushadidia kile ambacho kimekuwa kikizungumzwa dhidi yake.

[2]Mezger, S. (2002). Roman Catholic Faith Represented in Kezilahabi's *Mzingile*.
Rettova, A. (2004). Afrophone Philosophies: Posibilities and Practice. The Reflexion of Philosophical Influences in Euphrase Kezilahabi's *Nagona* and *Mzingile*.

## 2. 0 Dhana ya Dini

Katika utangulizi alioutoa Nkwera (1977: ix-xi) katika kitabu cha tamthiliya ya *Aliyeonja Pepo* kilichoandikwa na Farouk Topan, anasema, hapo zamani nyenzo iliyokuwa ikitegemewa sana ilikuwa ni dini. Dini ilimsaidia mwanadamu kutambua kuwa vitu vyote vilivyopo kama mito, radi, mvua, ndege, wanyama, samaki na pia yeye mwenyewe alitokana na nini au alitoka wapi. Anaendelea kwa kusema kuwa, mafunzo ya dini yalisaidia kuondoa migogoro mingi iliyokuwepo kama vile mapigano, vita na watu kuuana. Kwa hiyo, dini ilikuwa na nafasi ya kuwaunganisha watu. Aidha, anaitazama dini kama kitu cha mtu binafsi kitu ambacho ni cha itikadi na imani. Katika kumalizia, Nkwera anatuambia kuwa, madhumuni ya dini ni kumfanya mwanadamu aishi vema hapa duniani ili baada ya kifo aingie peponi huko ahera.

Kwa upande wa Omari (1981: 39-40), yeye anaitazama dini kama mfumo wa kiitakadi, viashirisho na matendo, mambo na vitu ambavyo hueleweka na kutambulika kwa njia ya imani na si kwa njia ya utafiti wa kitaaluma. Zaidi, dini ni lazima imhusishe mwanadamu na Mungu au viumbe vingine viishivyo ambavyo huaminika kuwa vinayo mamlaka kuliko mwanadamu, na maisha ya baada ya kufa na ulimwengu ujao, mambo ambayo hayafahamiki kitaaluma, kiutafiti au kutawaliwa nayo.

Kwa kupitia maelezo ya wataalamu hao, hapana shaka kuwa dini ni chombo cha kiitikadi au kiimani ambacho kinafungamanishwa na imani ya kuwepo pepo au mbingu; mahali ambapo ni watenda mema tu ndio watakaostahili kuingia. Vile vile, dini inaonekana kuwa na nafasi muhimu katika jamii.

## 3.0 Jinsi Suala la Dini Linavyojitokeza katika Vitabu Husika vya Fasihi

### 3.1 *The Black Hermit* (Mtawa Mweusi)

Mtunzi wa tamthiliya hii ni Ngugi wa Thiong’o (1993). The *Black Hermit* ni tamthiliya inayomzungukia mhusika mkuu Remi. Remi alikuwa ni msomi ambaye jamii yake ilimtegemea sana yeye aisimamie na kuiongoza. Mhusika huyu analazimika kukimbilia mjini kutokana na mambo makubwa matatu.
Jambo la kwanza, anakataa kuwawakilisha wanajamii wake kutokana na kile anachodai kuwa jamii yake imegubikwa na ukabila wa hali ya juu.

Pili, anakimbilia mjini baada ya kutakiwa kumrithi mke wa marehemu kaka yake aliyeitwa Muthoni na utaratibu huu ulitokana na mila na desturi za jamii yake. Jambo la tatu ambalo ndilo kiini cha uchambuzi wa kazi hii limejikita katika suala zima la dini, ambapo tunaambiwa kuwa kuwepo kwa dini ya Kikristo katika jamii ya Remi kumeleta athari kubwa. Katika dini hii ya Ukristo Pasta ndiye alikuwa

kiongozi mkuu wa dini ya Kikristo. Dini hii ya Kikristo inaonekana kuleta mgawanyiko kwa jamii inayosawiriwa katika tamthiliya hii.

Remi pia, alikimbia kutoka kwenye jamii yake ambapo Pasta alikuwa ni mzee sana na alitarajia kwamba Remi ndiye mtu pekee ambaye angeweza kuziba nafasi yake. Baada ya Remi kukimbilia mjini, mama yake ajulikanaye kama Nyobi aliamini kuwa ni nguvu ya Kristo pekee ndiyo itakayoweza kumrudisha Remi kutoka mjini alikokuwa amekimbilia hadi nyumbani (uk.18).

Mwandishi anatuonesha kuwepo kwa misigano ya kimitazamo kuhusu suala hili la dini. Wakati ambapo mama yake Remi na Pasta wanaamini kuwa dini ndicho chombo pekee kinachoweza kumrudisha Remi kwa nguvu za Kristo. Remi mwenyewe anaitazama dini kama chombo ambacho hakina manufaa yoyote katika jamii. Remi anasema:

> Pasta, wewe na dini yako hamjafanya kitu chochote kwa watu wetu. Zaidi imewagawanya watu na kuwadhoofisha hata kabla ya kuja kwa mzungu (uk.74).

Hivyo basi, tunaweza kuona kuwa mwandishi wa kazi hii kwa kupitia maelezo hayo, anaiona dini kama chombo kisichokuwa na nafasi muhimu zaidi ya kusababisha mgawanyiko baina ya wenyeji. Anayaonesha haya kwa kupitia mhusika mkuu Remi ambaye yeye anaiona dini kama kitu chenye athari ya kuwagawa watu na kuwadhoofisha. Itakumbukwa kuwa mgawanyiko huu wa watu uliwadhoofisha katika kipindi ambacho kilikuwa ni muhimu sana, kipindi ambacho watu walihitaji kuwa kitu kimoja lakini dini ikawa chanzo cha kudhoofisha umoja wa jamii hii.

### 3.2 *Aliyeonja Pepo*

Aliyeonja Pepo ni miongoni mwa kazi za tamthiliya zilizotungwa na Farouk M. Topan na kuchapishwa mwaka (1977).
Sehemu kubwa ya kazi hii ya *Aliyeonja Pepo* ina mazingira ya dini na maisha ya ulimwengu ujao. Mwandishi huyu anatumia mbinu ya mzaha kuonyesha udhaifu uliopo katika taratibu za mbinguni. Usawiri wa majina ya wahusika yaani, Juma Hamisi, Ziraili na Jiburili ni dhahiri kuwa yanadhihirisha usawiri wa imani ya dini ya Kiislamu.

Katika sura nyingine mwandishi huyu anatoa mafunzo kuhusu maisha ya peponi na anaitazama pepo kama mahali ambapo ni wale watakaotenda mema tu ndio watakaoingia peponi. Vile vile, kuwepo kwa pepo hii kunaonyeshwa kupitia kwa

mhusika Bwana Juma Hamisi ambaye alikuwa ni mkazi wa Bagamoyo akijishughulisha na shughuli za uvuvi. Tunaona kuwa Juma Hamisi anatolewa roho yake na kupelekwa peponi kazi iliyofanyika kwa makosa kwani yeye alitakiwa kwenda peponi baada ya mwaka mmoja na hivyo roho yake kuchukuliwa kimakosa.

Pia, kosa hili linamshughulisha vilivyo malaika mtoa roho na kuamini kuwa shetani ndiye aliyeingilia kati na hivyo kosa hili kufanyika:

ZIRAILI: Lakini namjua aliyetupotosha hivi.
JIBURILI: Nani?
ZIRAILI: Yule Ibilisi. Hii kazi yake. Kazi ya shetani hii. Nikikumbana naye atakiona.
Atakiona kilichomtoa kanga manyonya (uk.9).

Kutokana na majibizano hayo hapo juu, mwandishi huyu anatuibulia jambo la tafakari kuwa kumbe yawezekana si kila kifo husababishwa na Mungu bali wakati mwingine shetani huingilia kati na kutoa roho za watu. Dhana hii inaweza kutazamwa kama sehemu ya kejeli inayojaribu kuonesha udhaifu wa kiutendaji unaofanywa na malaika huko mbinguni kuwa ni sawa na udhaifu wa kiutendaji unaofanywa na wanadamu. Kutokana na kosa hilo lililofanywa na malaika mtoa roho, bwana Juma Hamisi wa Bagamoyo anatakiwa arudi tena duniani na asubiri mwaka mzima ndipo aweze kurudi tena peponi. John Hounington wa Uingereza ambaye alikuwa ni Mkristo ndiye haswa aliyepaswa kuingia peponi na sio bwana Juma Hamisi wa Bagamoyo.

Kadhalika, tamthiliya hii inaonyesha kuwepo kwa dini mbili tofauti yaani Ukristo na Uislamu ambazo kwa hakika haziingiliani. Mwandishi huyu anaonyesha tofauti hii pale ambapo Juma Hamisi ambaye ni Mwislamu anatakiwa arudi duniani huko Uingereza avishwe mwili wa bwana John Hounington ambaye ndiye aliyestahili hasa kuingia peponi badala ya Juma Hamisi. Ugumu unajitokeza pale ambapo John Hounington anakunywa pombe, anafuga mbwa na kula nguruwe vitu hivi vyote vikiwa ni haramu kwa bwana Juma Hamisi ambaye ni Mwislamu. Ni kutokana na tofauti hizi za kiimani ndizo zinazofanya Juma Hamisi akatae roho yake kuwekwa ndani ya mwili wa John Hounington.

Kubwa zaidi alilotaka kuonesha mwandishi huyu ilikuwa ni kuonesha kuwepo kwa pepo kwa wale watenda mema. Peponi anapatazama kama mahali ambapo kuna maisha ya raha, hamna dhambi, hamna mambo ya wivu wala mimba. Pia, kuna wanawake wazuri ambao huwastarehesha watu wanaoingia peponi na hii ndio sababu iliyomfanya Juma Hamisi asikubali kurudi duniani. Hii inadhihirishwa na majibizano yaliyokuwapo kati ya bwana Juma Hamisi na Ziraili.

JUMA: Mahali pa starehe hapa

ZIRAILI: Ndio maana pakaitwa peponi (uk.12).

Hapana shaka kwamba starehe na maisha ya raha mustarehe aliyoyaonja bwana Juma Hamisi ndio yaliyomfanya asikubali kurudi tena duniani. Hivyo ndivyo Topan anavyopasawiri peponi kwa kupiti tamthiliya yake hiyo ya *Aliyeonja Pepo*.

**3.3 *Rosa Mistika***

Katika riwaya hii ya *Rosa Mistika*, mwandishi Euphrase Kezilahabi (1988) ametumia jina hili la kitabu kusawiri dini hususani dini ya Kikristo, dhehebu la Kikatoliki ambapo ni fumbo la waridi lenye kumaanisha Bikra Maria. *Rosa Mistika* ni riwaya inayomsawiri Rosa ambaye alikuwa ndiye mhusika mkuu. Mhusika huyu anapewa sifa za kila namna na mwandishi. Akiwa mtoto wa kwanza kwenye familia yake anakulia katika mazingira magumu sana si tu kimaisha bali pia hata kimalezi. Baba yake Rosa alipenda sana kutumia ukali kama njia ya kuleta malezi mema kwa watoto wake. Hali hii iliwafanya watoto wake (hasa Zakaria) kuwa na tabia mbaya zaidi pindi alipokuwa katika mazingira ya mbali na nyumbani.

Dhana ya dini imeweza kujitokeza kwanza katika kusawiri jina la kitabu yaani *Rosa Mistika*. Pia, suala la dini limeoneshwa kupitia kwa masista waliokuwa wakiishi Kagunguli ambao pia mchango wao katika jamii umeonyeshwa pale tu Flora mdogo wa marehemu Rosa anapowaomba masista hawa wamsaidie kuwatunza dada zake kwa muda wa miaka miwili. Mwandishi anasema:

Baada ya ndugu kugawana vitu vyote… Flora aliwaomba masista waliokuwa wakikaa Kagunguli wamsaidie kutunza dada zake kwa muda wa miaka miwili, hawakukataa, walimwonea huruma (uk. 96).

Pia, dini inaonyeshwa kupitia kwa Charles ambaye alikwenda Kisubi kusomea ubruda. Huyu alichagua kuishi maisha ya bila kuoa (uk. 97).

Aidha, dini imeweza kuoneshwa kupitia ibada ya mazishi inayofanywa na Padri katika mazishi ya Zakaria na mkewe.

Mbali namwandishi huyu kuisawiri dini kama chombo chenye mchango chanya katika jamii bado anaiona dini kama chombo ambacho hakina manufaa yoyote kwa jamii hususani katika kuleta au kumkomboa mtu ambaye ameshaharibika kitabia. Mwandishi anamtumia Padri ambaye anakwenda kwa Rosa kumpelekea habari njema ili aweze kuachana na matendo yake maovu lakini tunaonyeshwa anashindwa na anaondoka bila mafanikio yoyote huku Rosa akiendelea na tabia za kutoa mimba na kutembea na waume za watu akiwemo mkuu wake wa chuo mpaka pale alipokuja kushambuliwa na kuumizwa vibaya na mke wa mkuu huyo

wa chuo (kur. 48-49). Mwandishi anamuonesha Padri aliyekwenda kwa Rosa kumpelekea neno la Mungu. Anasema:

Rosa, nimekuja kukusaidia wewe maskini wa roho, mwovu huonekana kwa matendo.

Mimi mtumishi wa Mungu, nimekuletea habari njema (kur. 48-49).

Licha ya jitihada hizo zilizofanywa na Padri za kumtaka Rosa aachane na matendo yake mabaya na amrudie Mungu, lakini jitihada hizo zinagonga mwamba. Mwandishi anasema:

Wokovu! Wokovu gani! Kama kuna moto basi nitakwenda (uk. 49).

Maelezo haya bado yanatuacha njia panda hususani pale tunapojiuliza iwapo dini ina nafasi kubwa katika kufanikisha kumrudi mtu ambaye tayari amekwishapotoka kimaadili.

### 3.4 *Kwenye Ukingo wa Thim*

Tamthiliya hii ya kwenye *Ukingo wa Thim* iliandikwa na Ebrahim Hussein (1997). Katika tamthiliya hii ya *Kwenye Ukingo wa Thim* mwandishi huyu alikusudia sana kuonyesha mvutano mkubwa uliopo hasa wa kitamaduni unaosababishwa na kuendeleza ukabila. Suala hili linawaathiri sana wanandoa wawili kutoka makabila mawili tofauti ambao ni Herbert Palla na mkewe Martha. Hawa wanatengwa na ndugu zao baada ya kuoana.

Mgogoro mkubwa unazuka pale Herbert Palla anapofariki na mkewe kuzuiliwa kumzika mumewe. Hali hii haishii hapa tu, bali pia inasababisha *Umma Clan* kuvamia nyumba ya wana ndoa hawa wawili kwa kuishambulia kwa mawe na kuvunja vioo na tena wanamnyamnyasa mjane huyu kwa kumnyang'anya mali zote alizochuma na mumewe. Ni katika dhuluma hii ndipo suala la dini linapoweza kusawiriwa na mwandishi.

Dhana hii ya dini inaonyeshwa na mwandishi kama chombo kisichokuwa na manufaa yoyote kwa jamii kwani inatumika kama chombo cha kuendeleza unyanyasaji, ukandamizaji na unyonyaji katika jamii. Mwandishi anatuthibitishia haya (kur. 30-32);

PASTA: Wewe huwezi kujua la kufanya. Mwachie Mungu.

PASTA: Unakumbuka uliponunua nyumba hii, bustani hizi, ulijiona umefika. Sasa aliyekupa vyote hivi amevichukua (*Martha anazidi kulia*)

PASTA: Hii ni kazi ya Mungu na kazi ya Mungu haina makosa.

Hii inaonyesha kuwa dini inatumika katika jamii kama chombo cha kuendeleza mfumo kandamizi na kumnyima mwanamke haki ya kumiliki mali halali aliyochuma na mumewe. Itakumbukwa kuwa, Martha alitaka kuilinda mali yake aliyoichuma na mumewe kwa kutumia bunduki lakini Pasta alimzuia asiitumie

bunduki ile na hatimaye *Umma Clan* wakachukua mali zake zote alizokuwa amechuma na mume wake:

George anashuka ngazi mbio. Ameshika hati mkononi. Martha anachukua bunduki. Anamlenga George.

PASTA: Martha! Mlaani shetani (uk. 32).

Hivi ndivyo mwandishi Ebrahim Hussein anavyokisawiri kipengele cha dini katika tamthiliya hii ya *Kwenye Ukingo wa Thim*.

### 3.5 *Mfalme Juha*

Hii pia ni tamthiliya nyingine ya mwandishi Farouk M. Topan (1971). Tamthiliya hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inaonesha pale mfalme anapopitisha sheria yake ya kila kitu kipimwe ratili moja kwa pesa moja. Sehemu ya pili inazungumzia athari za sheria hiyo ambapo yanatokea mashtaka mbalimbali ambayo zaidi yanahusishwa na kuanzishwa kwa sheria hiyo. Sehemu ya tatu na ya mwisho ni ile inayosawiri jina la kitabu *Mfalme Juha* pale anapojitangazia kunyongwa badala ya Bakari ikiwa ni athari ya masuala ya kiimani yatokanayo na mafundisho ya dini katika jamii.

Mwandishi huyu ametumia mji wa Kichaa kuwa ni mji unaoongozwa na Mfalme Juha ambaye anajilimbikizia madaraka yote na hivyo kushindwa kufanya maamuzi ya busara. Mfalme huyu ndiye hakimu na mtawala wa mji huu wa Kichaa. Matatizo mengi yanaibuka pale anapopitisha sheria kuwa kila kitu kipimwe ratili moja na kiuzwe kwa pesa moja. Ni kutokana na kupitishwa kwa sheria hii ndipo hata hatimaye mwishoni athari za namna mafundisho ya dini yanavyoweza kusababisha watu kujitolea kufa au kunyongwa ili waende peponi yanapojitokeza.
Athari za mafundisho ya dini katika jamii zinajitokeza pale ambapo Bakari ambaye alikuwa mtu mnene sana anasadikiwa kuwaua vijana watatu. Tukio hili linatokea pale Bakari ambaye alikuwa mnene sana anapopita katika sehemu ilipokuwa inajengwa nyumba ya Burahimu. Kutokana na unene wake aliwashangaza mafundi waliokuwa wakijenga nyumba hiyo wakashindwa kujenga vizuri na hatimaye kusababisha vifo vya vijana watatu waliotaka kuiba mali ya Burahimu na hatimaye kuangukiwa na nyumba hiyo.

Aidha, katika mashtaka haya, Bakari anatiwa nguvuni lakini kabla ya hukumu yake, Bawabu anamfikishia taarifa Walii ambaye alikuwa mwalimu wa Bakari. Walii anatumia dini katika kumwokoa Bakari kwa kumpumbaza na kumdanganya Mfalme Juha kuwa mtu yeyote atakayenyongwa mwezi mosi, mfungo tano, saa sita za mchana atakwenda peponi:

WALII: Kwa sababu, bwana, nitakwenda peponi moja kwa moja. Nimesoma kitabuni mtu yeyote atakayenyongwa leo mwezi mosi, mfungo tano, saa sita za mchana atakwenda peponi tu. Vile vile, imeandikwa kama mtu huyo akishafika peponi atapokelewa na malaika na atapewa nchi ya kutawala. Jumba lake litakuwa la dhahabu na kila kitu humo ndani kitakuwa cha dhahabu. Kila sanaa utaipata ndani ya nyumba hiyo. Masiti wazuri ajabu wenye macho meusi yaliyopakwa wanja wa kupendeza ambao ni wazuri hata hapa duniani hawapo watakuwa wakikupepea huku wakizungumza na wewe na kukuimbia mashairi kwa sauti nzuri. (uk. 31)

Azma hii ya kupasifia peponi inaendelea kushadidiwa kuwa atakayeingia peponi ni mtu yule anyongwaye badala ya mwenzie. Ni kutokana na maelezo haya yanayosadikiwa kutokana na mafundisho ya dini ndiyo yanayomfanya Mfalme Juha ajitangazie yeye kunyongwa badala ya Bakari. Hivyo, Mfalme Juha anasema kuwa atanyongwa yeye ili aweze kwenda peponi ili akakutane na mabibi wazuri:

MFALME JUHA: Leo usiku mabibi zangu wa peponi wataliimba shairi langu. Na mimi nitawapigia udi (uk. 33).

Kwa maelezo na mifano hiyo, tunaweza kuona ni kwa namna gani dini isipotumiwa vizuri inaweza kusababisha watu kujitangazia kunyongwa kwa niaba ya watu wengine.

**3.6 *Things Fall Apart* (Shujaa Okonkwo)**

Sehemu kubwa ya riwaya hii iliyoandikwa na Chinua Achebe na kuchapishwa mwaka 2000 imejaribu kuangalia maisha ya jamii ya watu wa Ibo katika kijiji kikubwa cha Umuofia. Maisha haya yameangaliwa kwa kutazama kipindi cha kabla ya ujio wa wageni/wazungu na pia maisha baada ya ujio wa wazungu. Kabla ya ujio wa wageni hawa, jamii ya mhusika mkuu Okonkwo na rafiki yake Obierika iliishi katika misingi ya mila, desturi na tamaduni ilizokuwa imejiwekea. Katika kulitazama hili, jamii hii ilikuwa na miungu na kati ya miungu hii alikuwepo mungu wa ardhi (*goddess of the earth*).

Pia, kuwepo kwa miungu hii kama inavyoonyeshwa kwa mungu wa ardhi, watu waliishi kwa amani ambapo pia walijaliwa baraka za kupata mavuno mema (uk. 22). Mbali na mungu wa ardhi, ilikuwepo miungu ya milimani na mapangoni. Lakini jamii hii kwa kupitia dini ya asili iliwatenga watu wa tabaka fulani ambao walijulikana kama Osu. Watu hawa hawakutakiwa kunyoa nywele kwani iliaminika kuwa watakaponyoa nywele zao watakufa. Pia, watu hawa hawakuruhusiwa kuchangamana na watu wa kawaida wala kuoa au kuolewa na watu wa kawaida. Pindi walipokufa, walitupwa katika Msitu wa maovu (*Evil forest*).

Kadhalika, tabaka jingine lililoumia kutokana na taratibu za jamii hii lilikuwa ni lile la watoto mapacha. Hawa, walitazamwa kama mkosi katika familia hivyo hawakuruhusiwa kukua bali pindi tu walipozaliwa walitupwa kwenye msitu wa maovu.

Dini/imani iliongoza mambo mbalimbali kama vile kuwepo kwa wiki ya amani (*Week of peace*). Katika kipindi hiki, ilikuwa ni makosa kumpiga mtu mwingine na kitendo hiki cha kupiga kilisababisha mhusika kupewa adhabu. Okonkwo anakiuka mwiko huu kwa kumpiga mke wake baada ya kufika nyumbani na kutomkuta mke wake wa tatu. Hivyo, aliadhibiwa kwa amri kutoka kwa mungu wa ardhi (*goddess of the earth*) kwani kwa kukiuka masharti ya wiki hii ambayo ilikuwa ni wiki moja kabla ya kupanda mazao kungesababisha ardhi kutozalisha mazao ya kutosha.

Dini ya Kikristo ambayo inaingia Mbanta na baadaye Umuofia ilikuwa na athari kubwa katika jamii. Dini hii ya Kikristo inamkuta Okonkwo akiwa kizuizini Mbanta baada ya kumuua kijana mmoja kwa bahati mbaya katika mazishi ya Ezeudu; mzee aliyekuwa maarufu sana katika Umuofia (uk.84).
Dini hii ya Kikristo huko Mbanta inahubiri kuwa watu wema wanaomwabudu Mungu wa kweli huishi milele katika ufalme wa furaha wa Mungu (uk.102). Mbali na mafundisho hayo ya dini yaliyohubiri kuhusu suala la kuwapo kwa Mungu mmoja na mwanae wa pekee aitwae Kristo, athari hasi za dini zinaanza kujitokeza hasa pale dini inapoanza kuleta mgawanyiko katika jamii hasa pale baadhi ya wenyeji wanapoamua kujiunga na dini hii ya Kikristo. Mfano mzuri ni Nwoye ambaye ni mtoto wa Okonkwo. Huyu anavutiwa sana na mahubiri yanayotolewa hasa yale yanayosisitiza upendo yaani watu kupendana na kupinga suala la mauaji ya watoto mapacha na pia mauaji kama yaliyofanywa kwa rafiki yake Nwoye aliyejulikana kama Ikemefuna. Ikemefuna aliuawa kwa agizo la miungu iliyokuwa inaabudiwa na jamii hiyo.

Baada ya Okonkwo kusikia kuwa mwanaye Nwoye alikuwa kwenye mahubiri ya dini hii mpya alimchapa sana. Kitendo hiki kinamfanya Nwoye akimbie nyumbani na kujiunga na Wakristo hawa moja kwa moja na hatimaye kuhama nyumbani jumla.

Vile vile, dini/kanisa inawakusanya watoto ambao walikuwa wametupwa kwenye msitu wa maovu na kuwalea kanisani na pia inawapokea ma-Osu na kuwafanya kuwa waumini. Kitendo hiki kinawachukiza sana akina Okonkwo na watu wengine wenye msimamo kuhusu dini yao ya asili.

Athari za dini ya Kikristo katika jamii hii ya Umuofia inaonekana pale Okoli ambaye alikuwa ni Osu mmojawapo anapomuua Chatu aliyekuwa akiheshimiwa sana na wana Umuofia (*sacred python*) (uk.114). Baada ya kumuua chatu huyu, Okoli alifariki na hii ikadhihirisha kuwa miungu yao bado ilikuwa ikiwapigania. Tukio la Okoli kuaminika kumuua nyoka huyo lilisababisha waumini hawa kuzuiliwa hata kwenda kuchota maji katika sehemu zilizokuwa zikitumiwa na wana jamii.

Hatimaye, unazuka ugomvi mkubwa pale ambapo wazee wa kimila walipokuwa katika mchezo wa maadhimisho ya sherehe ya kimila na muumini mmoja wa dini ya Kikristo kwenda kumvua kinyago mzee mmojawapo kitu ambacho kilikuwa ni mwiko mkubwa. Hapa, wazee wa jamii hiyo wanaamua kwenda kuchoma kanisa hili la Kikristo. Kutokana na kuwepo mwingiliano kati ya dini, utawala na nguvu ya dola, Mkuu wa wilaya anawakamata viongozi watano wa kimila akiwemo Okonkwo na kuwapa mateso makali na kisha kuamuru kwamba ni lazima walipe fidia kwa mfumo wa magunia mia mbili hamsini ya nafaka ndipo waweze kuachiliwa (uk.139).

Kwa ufupi, katika kitabu hiki tunaona kuwa jamii inagawanyika baada ya kuingia kwa dini ya Kikristo, dini ambayo ilikuwa inasimamiwa na utawala wa kigeni kwa kutumia nguvu ya dola. Tukio la mhusika mkuu kujiua kwa kujinyonga linafungamanishwa chanzo chake katika mivutano kiimani.

## 4.0 Mjadala

Waandishi wote katika kazi zao wamefanana katika kuonesha kuwapo kwa suala la dini katika jamii licha ya kutofautiana kwao ambapo suala hili wameliegemeza katika dini ya Kiislamu na wengine katika dini ya Kikristo. Pia, wameonesha dhahiri kuwapo kwa imani inayoegemezwa kwa Mungu au miungu ambayo kimsingi inaaminiwa kuwa na nguvu kuliko mwanadamu[3].

Topan katika kazi zake zote mbili na Chinua Achebe, wao wameonesha moja kwa moja katika kazi zao kuwa watu watakaokwenda peponi ni wale tu watakaokuwa wametenda mema. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa waandishi wengine waliobaki wanakanusha suala la kuwepo kwa pepo kwa wale watakaotenda mema tu, hasa tukizingatia mafundisho yote ya dini hizi yaani Uislamu na Ukristo daima yanawasisitiza watu kutenda mema ili waweze kwenda peponi.[4] Aidha, Kezilahabi

[3] Omari (1981:41) anadai kuwa mwanadamu ameumbwa na mwingine ambaye ni mkubwa kumshinda mwanadamu mwenyewe…

[4] Mulokozi (1999) (Mh.) katika *Utenzi wa Mwanakupona* naye anathibitisha suala la kuwepo kwa pepo kwa wale watakao tenda mema na ndio maana Mwanakupona Binti Mshamu katika utenzi huu anamuasa binti Mwana Hashima Binti Mataka kumtii mumewe ili atakapokufa aende peponi.

kama ilivyo kwa Topan, anatuambia kuwa ili mtu aingie peponi ni sharti afe kwanza, na ndio maana hata katika riwaya yake ya *Rosa Mistika*, anatuonesha kuwa baada ya Rosa na Zakaria kufariki ndipo wanapofika mbinguni napo wanakutana na Mungu ambaye anafanya mahojiano nao wote wawili ili aweze kutoa hukumu.

Topan anatuambia kuwa kwa wale watakaotenda mema watakutana na masiti wazuri ambapo mtu atakuwa na fursa ya kuchagua siti yeyote wa kustarehe naye. Mawazo haya yanapingana na yale yanayopatikana katika Biblia Takatifu yanayotuambia kuwa mbinguni hapana suala la kuoa au kuolewa. Usawiri huu wa Topan unatuibulia changamoto nzito sana hususani pale tunapojaribu kujadili peponi ni sehemu gani? Pengine, udhahania wa kuwepo kwa peponi; mahali ambapo hatuna ushahidi yakinifu wa kuwepo kwake kwa maana hapana mtu aliyewahi kujitokeza na kuthibitisha kuwepo kwa pepo ambayo pengine yeye amewahi kufika huko ndiyo sababu ya kutuacha na maswali haya.

Fauka na hayo, kazi hizo za fasihi licha kujaribu kuisawiri dini kama asasi inayoweza kuleta maendeleo kwa jamii, bado dini inaonekana kuwa na athari hasi katika jamii. Kuwepo kwa athari hasi kunatukumbusha ule msemo wa wahenga usemao, ‘Hapana kizuri kisichokuwa na dosari.’ Usawiri huu wa dini katika kazi hizi za fasihi pengine unatukumbusha mawazo ya baadhi ya wanafalsafa kuwa huwa hakuna asasi timilifu kwa asilimia mia moja na hivyo, ili kuupata ukamilifu hatuna budi kuchangamanisha mafunzo yanayotokana na asasi mbalimbali.

Kwa mfano, dini imeweza kutazamwa kama asasi inayoweza kusababisha maangamizi, kuleta utengano katika jamii, kuhalalisha ukandamizaji, unyonyaji na unyanyasaji pale isipotumiwa vizuri. Tena, yawezekana dini isiwe na uwezo wa kumrudisha kwenye mstari mtu ambaye tayari amekwishapotoka kimaadili. Mfalme Juha anajitolea kunyongwa kwa niaba ya Bakari baada ya kuambiwa vitabu vya dini vinasema mtu atakayenyongwa kwa niaba ya mwenzake basi atakwenda peponi. Martha anadhulumiwa mali alizochuma na mume wake na anapotaka kutumia bunduki kulinda mali zake Pasta anamzuia na baadae anamwambia aliyekupa mali leo amezichukua. Achebe anatuonesha kuwa dini ya Kikristo ilisababisha jamii ya wana Umuofia kutengana na hivyo umoja wao ukavunjika kutokana na ujio huo wa wageni. Usawiri huo umechukuana na ule wa Ngugi anayetuambia ujio wa Pasta na dini yake ulikuja kuwagawanya watu katika kipindi muhimu kabisa cha kupigania uhuru. Kezilahabi kwa kupitia kwa Padri anatuonesha kuwa dini haina nafasi ya kuweza kumrudi mtu ambaye tayari alikuwa amekwishapotoka kimaadili.

Yawezekana kupitia usawiri huu wa suala la dini katika kazi za fasihi, ipo haja ya kuyachunguza upya mafundisho ya dini na ikiwezekana kuyabadilisha ili yachukuane na hali halisi au mabadiliko ya jamii husika.

**4.0 Hitimisho**

Makala haya yamejaribu kuchambua jinsi suala la dini linavyosawiriwa katika kazi za fasihi za waandishi watano huku ikilenga maswali makuu mawili; Ni ipi nafasi ya dini kwa mwanadamu? Na je, ni kweli dini ni asasi timilifu kama ambavyo imekuwa ikichukuliwa na wanajamii? Majibu ya maswali haya yanapatikana kutokana na mjadala uliooneshwa katika sehemu iliyotangulia. Kwa kupitia uchangamanishaji wa kazi hizo ni dhahiri kuwa makala haya yamejaribu kutufumbua macho juu ya dhana ya dini na pengine yamejaribu kutukumbusha kuwa hakuna kizuri kisichokuwa na dosari.

## Marejeleo

Achebe, C. (2000). *Things Fall Apart*, Nairobi: EAEP Ltd.

Hussein, E. (1997). *Kwenye Ukingo wa Thim*, Nairobi: Nairobi University Press.

Kezilahabi, E. (1975). *Rosa Mistika*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mezger, S. (2002). Roman Catholic Faith Represented in Kezilahabi's *Mzingile*. *Swahili Forum ix*, kur. 75-85

Mulokozi, M.M. (Mh.) (1999). *Tenzi Tatu za Kale*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Omari, C.K. na Mvungi, M. (Wah.) (1981). *Urithi wa Utamaduni Wetu*, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Topan, F.M. (1971). *Mfalme Juha*, Dar es Salaam: Oxford University Press.

(1977). *Aliyeonja Pepo*, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Wa Thiong'o, N. (1993). *The Black Hermit*, Nairobi: EAEP.